



MFUKO WA
UTAMADUNI NA
SANAA TANZANIA

Jengo la Utumishi,
Kitalu A, 8 Barabara ya Kivukoni,
11101 Kivukoni, Dar es Salaam.

0738 246 286 / 0738 246 315

 www.tacaf.go.tz

 mfuko.utamaduni@michezo.go.tz

   [mfukotamadunitz](#)



JAMHURIYA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA
(TACAF)



MFUKO WA
UTAMADUNI NA
SANAA TANZANIA

WAOMBAJI WA KAMPUNI

UTANGULIZI

Mfuko wa Utamaduni na sanaa umeanzishwa kwa sheria ya ujumuisho wa wadhamini (Trustees' incorporation Act) kama ilivyo rejelewa mwaka 2002 (CAP. 318 R.E.2002) na kupewa hati ya usajili yenye namba 1776 tarehe 30 sepemba, 2020.

LENGO LA MFUKO

Kuinua ubora wa kazi za utamaduni na sanaa ili ziweze kujiendesha kibiashara, kutengeneza ajira nchini pamoja na pato la Taifa.

SEKTA ZINAZO HUDUMIWA NA MFUKO

- Sanaa za Muziki - Taarabu, Injili, Singeli, Kizazi kipya, Kaswida, Hiphop, Muziki wa Dansi
- Sanaa za Filamu - Wazalishaji, Waandaaji wa Maudhui, waigizaji, wasambazaji, waongozaji, wapiga picha, waandishi wa miswada, wana mandhali
- Sanaa za Maonesho - Upambaji, Sarakasi, Upishi, Michezo ya Jukwaani, U-DJ, Ushereheshaji, Ngoma za Asili
- Sanaa za Ufundi - Utendengenzaji wa Batiki, Uchoraji, Ususi, uchongaji, Utendengezaji wa Shanga, Ubunifu wa mitindo, Uchoraji wa picha za Tingatinga
- Lugha na Fasihi - Waandishi wa vitabu, wasambazaji, watunzi wa mashairi

WALENGWA WA MFUKO

- Mtu Binafsi;
- Kikundi; na
- Kampuni

AINA YA HUDUMA ZA MKOPO

- a) Mikopo ya uendeshaji:
Kuendesha kazi za walengwa kama vile matamasha, mashindano, kutayarisha au kuzindua kazi za Utamaduni na Sanaa na shughuli zingine zinazofanana na hizo.
- b) Mikopo ya Vifaa
Kununua vifaa vya kazi vitakavyotumika katika kuzalisha kazi za Utamaduni na Sanaa.
- c) Mikopo ya kujikimu / Dharura
Mikopo ya muda mfupi kwa ajili ya kujikimu wakati wa safari za kuandaa au kufanikisha kazi za Utamaduni na Sanaa

VIGEZO VYA WANUFAIKA WA MKOPO KWA WAOMBAJI WA KAMPUNI

- Barua ya maombi ya mkopo;
- Ujazaji wa Fomu na ambatisho la Andiko la Mradi;
- Leseni ya Biashara na Usajili wa Kampuni;
- Uthibitisho wa Mlipa Kodi (TIN);
- Taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka mmoja;
- Maazimio ya Bodi/ Board Resolution kuhusu kukopa;
- Nakala ya mizania ya mwaka 'Annual Returns' iliyoidhinishwa na BRELA;
- Utambulisho wa makazi ya wakurugenzi na eneo la Biashara ya kampuni;
- Cheti cha usajili/Utambulisho/Kibali kutoka Taasisi inayosimamia kazi ya Utamaduni au Sanaa;
- Utambulisho wa Kampuni kuwa ni mwanachama wa Umoja wowote ikiwemo Shirikisho, Chama au kikundi kilichosajiliwa kisheria katika Sekta ya Utamaduni na Sanaa;
- Taarifa ya mauzo ya kazi za Sanaa kupitia Benki Statement au miamala ya simu; na
- Ankra Kifani (endapo mkopo ni wa vitendea kazi/Vifaa).

SIFA ZA MKOPO

- Kiwango cha Mkopo ni kuanzia TZS 200,000/= hadi TZS 100,000,000/=
- Muda wa Marejesho ni miezi 24 (Miaka 2).
- Riba ni asalimia tisa (9%).
- Muda wa rehema (grace period) ni miezi mitatu (3).

NAMNA YA KUWASILISHA MAOMBI

Maombi yote yatumwe kwa:
Afisa Mtendaji Mkuu,
Mfuko wa Utamaduni na Sanaa,
S.L.P 8031,
DAR ES SALAAM

Na kuwasilishwa kupitia:
Barua pepe: mfukoutamaduni@michezo.go.tz